

UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

BANK OF TANZANIA



*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. FA.377/433/01/406**

**25 Aprili 2024**

**Kwa: Watoa Huduma Ndogo za Fedha wa Daraja la Pili,**

**YAH: KUANZISHWA KWA MAFUNZO YA WELEDI WA KITAALUMA KATIKA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA (MICROFINANCE CERTIFICATION PROGRAMME)**

Tafadhali rejea kichwa cha sekula hapo juu.

2. Benki Kuu ya Tanzania imeanzisha mafunzo ya weledi wa kitaaluma kwa Watoa Huduma Ndogo za Fedha wa Daraja la Pili (*Microfinance Service Providers – Tier II*).
3. Lengo la mafunzo haya ni kuwajengea uwezo watoa huduma ndogo za fedha wa daraja la pili ili kuongeza elimu, ujuzi, ufanisi na maadili katika utoaji wa huduma. Mafunzo haya yatawawezesha watoa huduma ndogo za fedha daraja la pili kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali inayotolewa na Benki Kuu katika kusimamia biashara hizo.
4. Mafunzo haya ni endelevu na kwa awamu ya kwanza yanatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 10 hadi 21 Juni 2024 katika ukumbi wa Benki Kuu uliopo Ofisi Kuu Ndogo za Dar es Salaam.
5. Walengwa wa mafunzo haya ni wadau katika utoaji wa Huduma Ndogo za Fedha Daraja la Pili, yaani Wamiliki, Wakurugenzi wa Bodi, Menejimenti, Maafisa Mikopo, Wakaguzi

na Wahasibu . Pia Benki Kuu inawakaribisha Maafisa Tehama, Washauri Elekezi na watu wote watakaopenda kujifunza mafunzo haya. Gharama ya mafunzo kwa kila mshiriki ni TZS. 500,000/= na ilipwe kupitia akaunti namba:

Jina la Benki: **Benki Kuu ya Tanzania**  
Akaunti Namba: **9924191003**  
Jina la Akaunti: **Bank Draft Issued**  
SWIFT CODE: **TANZTZXXXX**

6. Tuma maombi kwa kujaza fomu inayopatikana katika tovuti ya Chuo cha Benki Kuu ya Tanzania <https://academy.bot.go.tz> au tutumie maombi yako kupitia barua pepe [academy@bot.go.tz](mailto:academy@bot.go.tz). Kwa taarifa zaidi wasiliana na Daniel Mkude kupitia Simu Na. 0769 085 002 au kwa barua pepe [dmconstantino@bot.go.tz](mailto:dmconstantino@bot.go.tz).

7. Kwa vile mafunzo haya ni endelevu, watoa Huduma Ndogo za Fedha ambao tayari wana leseni ya Benki Kuu wanapewa kipindi cha mpito (moratorium period) cha miaka mitatu (3) kuhakikisha kuwa mmojawapo wa wadau waliotajwa katika kipengele namba 5 hapo juu wanapata mafunzo haya bila kukosa.

8. Kielelezo kuhusu mafunzo haya kimeambatanishwa kwa rejea zaidi.

Wasalaam,  
**BENKI KUU YA TANZANIA**

**KURUGENZI YA USIMAMIZI WA SEKTA YA FEDHA**